**HOTUBA YA UFUNGUZI YA MHE. JAJI FRANCIS S K. MUTUNGI**

**MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

**KATIKA KIKAO KATI YA TBC NA VYAMA VYA SIASA KUHUSU NAFASI NA MAJUKUMU YA TBC KATIKA UCHAGUZI**

**TAREHE 02 JUNI 2025 – UKUMBI WA MULTIFUNCTIONAL – CONFUSIOUS**

**CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDSM)**

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Wawakilishi kutoka Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC),

Wawakilishi wa Taasisi mbalimbali,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Habari za asubuhi

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa kuitikia mwaliko wa kushiriki kikao hiki muhimu, ambacho kinalenga kujadili kwa pamoja nafasi ya Shirika la Utangazaji Tanzania kama chombo cha habari cha serikali katika kuelekea Uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Waheshimiwa,

Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ina wajibu wa kuhakikisha vyama vya siasa vinafuata misingi ya demokrasia, kuheshimu sheria, na kujenga siasa safi na za kistaarabu.

Katika kutekeleza jukumu hilo, tunatambua kuwa Vyombo vya Habari, na hususan TBC kama chombo cha umma, vina mchango mkubwa katika kujenga mazingira ya uchaguzi wa haki, huru, na wa amani.

TBC inabeba dhamana ya kuuhabarisha umma kwa uwiano na usawa kwa vyama vyote vya siasa bila upendeleo. Huu ni wajibu wa kikatiba, wa kiuadilifu, na wa kitaasisi.

Kadhalika, vyombo vingine vya habari, vya umma na binafsi vinapaswa kufuata misingi hii hii, kwa kuhakikisha vinaepuka kuripoti habari za uchaguzi kwa upendeleo, propaganda au uchochezi.

Katika mazingira ya sasa ya kidijitali, tunakumbana pia na changamoto kubwa ya matumizi mabaya ya akili mnemba (Artificial Intelligence) katika kuunda na kusambaza taarifa, pamoja na ongezeko la taarifa potofu (fake news) katika majukwaa ya mitandao ya kijamii.

Ni wajibu wetu sote na hususan vyombo vya habari kama TBC kujitofautisha na kuwa chanzo cha taarifa za ukweli, sahihi na za kuaminika. Tunahitaji kutumia teknolojia kwa manufaa ya jamii, na siyo kwa kupotosha au kueneza taharuki au kwa manufaa ya upande mmoja pekee.

Tunataka wananchi watutegemee. Watambue kuwa wakitaka taarifa sahihi za uchaguzi kutoka katika vyombo vya habari vya ndani, TBC iwe sehemu ya kwanza ya kukimbilia.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Napenda pia kusisitiza kuwa mnao wajibu mkubwa katika kuhakikisha kuwa vyama vyenu vinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria, kanuni, na katiba zenu, kuzingatia maadili, na kuheshimu nafasi za vyombo vya habari ni hatua muhimu ya kujenga siasa zenye tija kwa taifa. Vyama viwe mfano wa uadilifu, uwajibikaji, na mshikamano wa kitaifa.

Kwa kumalizia, ni matarajio yangu kuwa kikao hiki kitatoa fursa ya mazungumzo ya wazi na ya kujenga, yatakayosaidia kuboresha ushirikiano kati ya TBC, vyombo vingine vya habari, na Vyama vya Siasa kwa lengo moja kuu ambalo ni kuimarisha misingi ya demokrasia ya vyama vingi na Uchaguzi wa amani nchini.

Kwa heshima kubwa, natamka kuwa kikao hiki kimefunguliwa rasmi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Mungu ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mungu ibariki demokrasia yetu.